OFISI YA RAISI-TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA KYELA

SHULE YA SEKONDARI NYASA LAKE SHORE

S.L.P. 411

SIMU: 0784630505/0764630505

E-MAIL: nyasalakeshore@yahoo.com

Mwanafunzi: _____

S.L.P._____

KYELA.

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI NYASA LAKE SHORE.

1.0 Ninayo furaha kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha Kwanza katika Shule hii mwaka 2021. Shule ya Nyasa Lake shore ipo umbali wa kilomita 45 kutoka Kyela mjini, na ipo kata ya Matema mwambao mwa ziwa Nyasa. Usafiri wa basi Kyela mjini unapatikana katika kituo cha mabasi cha Kyela ambapo nauli kutoka Kyela – Matema ni sh. 3,000/=.

Shule itafunguliwa tarehe 11/01/2021 kwa wanafunzi wa kutwa na tarehe 10/01/2021 kwa wanafunzi wa hosteli na tarehe ya mwisho kuripoti ni tarehe 18/01/2021.

2.0. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

SARE ZA SHULE

(a) WASICHANA

(a) Sketi mbili (2) rangi ya bluu na khaki lazima ziwe ndefu sana, mshono uwe rinda box mbele na nyuma.

Kitambaa kimeambatanishwa zingatia rangi na aina ya kitambaa.

(b) Mashati mawili (2) meupe yenye mikono mifupi

(c) Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kamba na visigino vifupi

(d) Soksi nyeupe jozi mbili (2)

(e) Sweta rangi ya bluu ni hiari kwa mwanafunzi sio lazima

(f) Kwa wanafunzi wa kiislamu Hijabu ni nyeupe na bluu, zisizokuwa na ulembo

(b) WAVULANA

(a) Suruali mbili (2) rangi ya bluu na khaki isiwe simple jeans na iwe na rinda moja. Kitambaa kimeambatanishwa zingatia rangi na aina ya kitambaa.

(b) Mashati mawili (2) meupe yenye mikono mifupi

(c) Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kamba na visigino vifupi

(d) Soksi nyeupe jozi mbili (2)

(e) Sweta rangi ya bluu ni hiari kwa mwanafunzi sio lazima

2.2 VIFAA VYA MICHEZO

a) Track suit moja/Bukta rangi ya bluu

b) Raba jozi moja na soksi ndefu

c) T-shirt rangi ya bluu iliyokolea (dark blue) yenye kola, pia iwe na nembo ya shule. Inaweza kupatikana shuleni kwa sh. 10,000/=

2.3 VIFAA VYA TAALUMA NA USAFI WA MAZINGIRA

a) Counter Book 3Quire 10

b) Bunda moja la Karatasi A4 lenye karatasi 500 kwa ajili ya mitihani ya mara kwa mara.

c) Pen, penseli na mkebe

d) Spring file moja

e) Jembe lenye mpini na ndoo ya lita 10

3.0 MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUADHIBIWA VIKALI

(a) Kuchelewa kufika shuleni

(b) Kujificha vichakani au porini

(c) Kupaka rangi, wanja, kuvaa herein na mikufu

(d) Kupiga kelele darasani

(e) Kukaa bwenini wakati wa vipindi au kazi za nje bila kibali chochote

(f) Kutembelea majumba ya starehe

(g) Kwenda ovyo kwenye nyumba za watumishi bila kibali

(h) Kutokuwa na vifaa vya darasani

(i) Kutokuvaa sare ya shule iliyoruhusiwa ama kuvaa milegezo. Mwanafunzi atatakiwa kuvaa sare maalum wakati wa darasani na sare yake ya kuvaa nje ya darasa atakapokuwa nje ya darasa.

(j) Kutokufanya kazi uliyopewa na kiongozi, mwalimu au mtumishi yeyote

(k) Kutoonyesha heshima kwa wakubwa ambao wanaingia na kutoka ndani ya shule

(l) Kutokufanya usafi bwenini mfano kudeki, kusafisha vyoo, kutandika kitanda na kusafisha mazingira yanayozunguka shule

(m) Kutohudhuria shuleni bila ruhusa yoyote kutoka kwa mzazi.

4. MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE

(a) Wizi

(b) Uasherati, ubakaji na ushoga

(c) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya

(d) Makosa ya jinai

(e) Kupigana au kupiga

(f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma

(g) Kudharau bendera ya Taifa

(h) Kuoa au kuolewa

(i) Kupata mimba au kusababisha mimba ndani na nje ya shule

(j) Kutoa mimba

(k) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa shule au watu

(l) Kukataa adhabu kwa makusudi

(m) Kutoroka shule au kulala nje ya shule(kwa wanafunzi wa bweni) bila ruhusa

(n) Kuwa na simu ya mkononi shuleni

(o) Kutokuwepo shuleni bila ruhusa kwa muda wa siku 30 mfululizo.

(p) Kutoa lugha chafu kwa mwanafunzi mwenzako, walimu, walezi na jamii kwa ujumla

(q) Kusuka nywele. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni

(r) Kutokufanya mazoeziya darasani na mitihani ya ndani na nje ya shule.

5. HESHIMA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

(a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.

(b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule ni muhimu.

(c) Kutimiza kwa makini maandalio ya jioni

(d) Kuwahi katika kila shughuli za shule kulingana na ratiba

(e) Kufahamu mipaka ya shule na maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wa uanafunzi wako katika shule hii ni jambo la lazima.
(f) Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule
(g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
(h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote unapotakiwa.
(i) Vitu vya thamani kama vile pasi ya umeme, radio, camera, simu na vitu vya anasa haviruhusiwi shuleni (Ni marufuku mwanafunzi kuwa navyo)

6. VIAMBATANISHO NA FOMU MUHIMU

(a) Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa hospitali ya Serikali.
(b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi/mkataba wa kutoshiriki katika mgomo, fujo na makosa ya jinai.
(c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni kulipa ada, michango na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.
(d) Picha za Passport size (3) za mwanafunzi na picha (2) za mzazi/mlezi

NB: Unatakiwa kutii sheria, taratibu na kanuni za shule muda wote uwapo shuleni. Kutojua sheria za shule haitakuwa kinga ya kutokuchukuliwa hatua. Kwa kipindi chote utakachokuwa mwanafunzi wa shule hii utakuwa unawakilisha shule na popote pale utakapokuwa. Hivyo basi utovu wa nidhamu utakaofanya bila ya kujali mahali au wakati, uongozi wa shule utachukua hatua za kinidhamu zinazo stahili dhidi yako.

KARIBU SANA KATIKA SHULE YA SEKONDARI NYASA LAKE SHORE

.....
LUSAJO S. MWAKITALIMA
MKUU WA SHULE
SCHOOL MOTTO "IMPOSSIBLE IS POSSIBLE"

NYASA LAKESHORE SECONDARY SCHOOL

RE: REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION REPORT FOR STUDENT TO BE ENROLLED FOR STUDIES IN SECONDARY EDUCATION.

To the Medical Officer,

……

……

……

RE: Surname …….. Age…… Sex……..

Other name (s) ……..

Please examine the above named as to her/his fitness for studies.

A. PERSONAL HISTORY

Is the examinee suffering from any of the following? Indicate Yes or No.

1. Tuberculosis …… 14. Epilepsy ……
2. Pneumonia …….. 15. Deformity ……
3. Pleurisy …….. 16. Psychiatric……
4. Asthma…….. 17. Eye disorder……..
5. Rheumatic fever…… 18. Ear, Nose/Throat Disorder……..
6. Allergic disorder…… 19. Skin diseases……..
7. Heart disease…….. 20. Anemia……
8. Gastric or duodenal…….. 21. Gynaecological disorder……
9. Recurrent indigestion…….. 22. Malaria/other tropical Diseases……
10. Jaundice…….. 23. Major or Minor Operation……
11. Dysentery…… 24. Serious accidents……..
12. Varicose Veins…….. 25. Any other serious disorder……..
13. Diabetes……..

B. LABORATORY

1. Urine Albumin ……

Sugar……..

Lucocecytes……..

Bilharzias……..

2. Stool: Special emphasis on Hookworm or Bilharzias

3. Blood Examination: Hb Level……

(a) Neutrophils ……..

(b) Eosinophils ……..

(c) Basophils……..

(d) Lymphocytes ……..

(e) Monocytes……

(f) ESR……..

4. Serology: Widal test …… VDRL……

D. MEDICAL CERTIFICATE (To be completed by a Medical Officer)

I have examined the above named person and consider that *She/he is physically and mentally/not physically and mentally fit to be admitted for the full time course at your School. *Delete as necessary

…….. …….. …… …….. ……..

Name Signature Date Title Qualification

Address: ……

……

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS- TAMISEMI
HALMASHAURI YA WILAYA YA KYELA

Namba za simu:
Mkuu wa Shule 0784630505
Makamu Mkuu wa Shule 0755277349
Email: nyasalakeshore@yahoo.com

SHULE YA SEKONDARI NYASA LAKESHORE
S.L.P. 411,
KYELA.

MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI

Sehemu hii ijazwe na mwanafunzi:

1. Jina kamili la Mwanafunzi:……

2. (a) Tarehe ya kuzaliwa:……

   (b) Kijiji/Mtaa alipozaliwa……

3.(a) Dini:……

   (b) Dhehebu:……

4. (a) Ni raia wa Tanzania? (Jibu NDIYO au HAPANA)……

   (b) Kama siyo Mtanzania, taja uraia wako na ulete cheti cha uraia:……

5. (a) Darasa ulilomaliza:……

   (b) Shule ulikotoka:……

6. (a) Jina kamili la Baba/Mama/Mlezi:……

   (b) Anwani ya Mzazi/Mlezi:……

   (c) Namba ya simu ya Mzazi/Mlezi:……

7. (a) Mahali unapoishi:……

   (b) Ni umbali gani kutoka shuleni?.....

8. (a) Unaishi na nani? Taja jina lake kamili:……

   (b) Una uhusiano gani na huyo uliyemtaja?..... ……..

   (c) Unaishi katika nyumba ya kupanga? (Jibu NDIYO au HAPANA)……

9. Mzazi/Mlezi anafanya kazi gani?.....

10. Je una ndugu wa karibu mbali na mzazi/mlezi hapo juu? (Jibu NDIYO au HAPANA)……..

Kama ndiyo, anaitwa nani?.....uhusiano ……

Anaishi wapi…… Namba yake ya simu……..

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS- TAMISEMI
HALMASHAURI YA WILAYA YA KYELA

Namba za simu:
Mkuu wa Shule 0784630505
Makamu Mkuu wa Shule 0755277349
Email: nyasalakeshore@yahoo.com

SHULE YA SEKONDARI NYASA LAKESHORE
S.L.P. 411,
KYELA.

FOMU YA KUKUBALI

PICHA YA MWANAFUNZI

A. MWANAFUNZI

Mimi ……. ambaye ni mwanafunzi niliyechaguliwa kujiunga na shule ya sekondari Nyasa Lake shore , nakubali kuchukua nafasi niliyopewa ya kidato cha …… kuwa, nitatii na kufuata sheria, taratibu na kanuni zote za shule. Na ninaahidi kuwa sitashawishi wala kushiriki mgomo wowote wala kufanya fujo au makosa ya jinai.

…….. ……..

Sahihi ya Mwanafunzi Tarehe

PICHA YA MZAZI/MLEZI

B. MZAZI/MLEZI

Mimi …… Mzazi/Mlezi wa……

Nimeyasoma masharti yote ya mwanangu kujiunga na Shule ya Sekondari Nyasa Lake shore.

Ninakubali na kuahidi kuwa mwanangu atafuata na kutii masharti yote ya shule. Aidha naahidi kuwa nitawajibika kumlipia gharama ama kumpa mahitaji mwanangu pamoja na michango mbalimbali ya shule na nitakuwa tayari kushirikiana na shule pindi nitakapotakiwa kufanya hivyo.

…… ……..

Sahihi ya Mzazi/Mlezi Tarehe